**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

---

*(Kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023)*

Ofisi ya Bunge,
10, Barabara ya Morogoro
S.L.P. 941
40490 Tambukareli
**DODOMA** **APRILI, 2024**

# YALIYOMO

**YALIYOMO** ........ i

**ORODHA YA VIFUPISHO** ........ iii

**SEHEMU YA KWANZA** ........ 1

1.0 **UTANGULIZI** ........ 1

1.1 Maelezo ya Awali ........ 1

1.2 Muundo wa Taarifa ........ 1

1.3 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati ........ 2

**SEHEMU YA PILI** ........ 3

2.0 **UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2023/2024 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2024/2025** ........ 3

2.1 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji ........ 3

2.1.1 Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha Kwa Mwaka Wa Fedha 2023/2024 ........ 3

2.1.2 Hatua za Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ........ 5

2.1.3 Hatua zilizofikiwa katika Utekelezaji wa Bajeti ........ 7

2.2 Uchambuzi wa Mpango kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ........ 11

2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ........ 13

2.3.1 Uchambuzi wa Maduhuli ........ 13

2.3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida ........ 14

2.3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo ........ 14

**SEHEMU YA TATU** ........ 16

3.0 **MAONI NA USHAURI WA KAMATI** ........ 16

3.1 Maelezo ya Jumla ........ 16

3.2 Maoni na Ushauri ........ 16

3.2.1 Umaliziaji wa Maboma ya Shule na Zahanati ........ 16

3.2.2 Fedha kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu iliyoharibiwa na mvua nchini; ........ 17

3.2.3 Ushiriki wa wakandarasi wazawa katika utekelezaji wa miradi ........ 18

3.2.4 Uanzishwaji na uendeshwaji wa shule za msingi za michepuo wa Kiingereza.... 19

3.2.5 Utekelezaji wa wajibu wa Wadau wa Miradi ya Mendeleo kurudisha faida kwa Jamii (CSR) ....19
3.2.6 Mapato ya Halmashauri kutokana na biashara ya Kaboni ....20
3.2.7 Utunzaji wa Mazingira katika Halmashauri ....21
3.2.8 Uhuishaji wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali, Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Sheria ya Manunuzi ya Umma ....22
3.2.9 Taasisi za Serikali zinazofanya kazi na Halmashauri kuzingatia bajeti za Halmashauri 23
**SEHEMU YA NNE** ....24
4.0 **HITIMISHO** ....24
4.1 Shukurani ....24
4.2 Mwisho ....26

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **TAMISEMI** | : Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **OR – TAMISEMI** | : Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **MUSE** | : Mfumo wa Ulipaji Serikalini |
| **OPD** | : Out Patient Department |
| **TARURA** | : Tanzania Rural and Urban Roads Agency |
| **VEO** | : Village Executive Officer |
| **CAG** | : Cotroller and Auditor General |
| **MSD** | : Medical Stores Department |
| **EFD** | : Electronic Fiscal Devices |
| **CSR** | : Corprate Social Responsibility |
| **D by D** | : Decentralization by Devolution |
| **TEHAMA** | : Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu kuu nne kama ifuatavyo:-

(a) Sehemu ya Kwanza inayotoa maelezo ya awali, muundo wa Taarifa na Msingi wa Kamati kuripoti Bungeni Matokeo ya Uchambuzi wake.

(b) Sehemu ya Pili inayobainisha Uchambuzi wa Kamati kuhusu Hali ya Utekelezaji wa Bajeti, Mipango iliyopo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(c) Sehemu ya Tatu ambayo inabainisha maoni ya Kamati na Ushauri kutokana na maoni hayo.

(d) Sehemu ya Nne inayotimisha na kubainisha msimamo wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi

## 1.3 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuhusu msingi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kuwa yamefanyiwa uchambuzi na Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Sehemu ya Kumi na Nne ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 imeweka masharti kuhusu utaratibu wa Bajeti za Wizara ikiwemo Bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI, kufanyiwa kazi na Bunge leko Tukufu. Miongoni mwa masharti hayo ni Bajeti hiyo kufanyiwa uchambuzi na Kamati ya Bunge ya Tawla za Mikoa na Serikali za Mitaa. Naomba kulijilisha Bunge hili kuwa, Kamati ilifanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais TAMISEMI kama ilivyostahili.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2023/2024 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2024/2025

### 2.1 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji

#### 2.1.1 Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha Kwa Mwaka Wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, iliitaka Kamati kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa Fedha 2023/2024. Katika mwaka huo, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya **Shilingi 3,485,999,641,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea miradi ya elimu, miradi ya afya na miradi ya barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA). Miradi iliyotemblewa inatekelezwa katika sehemu mbalimbali za nchi ikiwemo mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga. Jumla ya miradi 13 ilitembelewa katika mikoa hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya ukaguzi na uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa miradi hiyo unenesha mambo yafuatayo:-

**(a) Upangaji wa Miradi katika Awamu**

**Mheshimiwa Spika**, Baadhi ya miradi imekuwa ikipangwa kutekelezwa katika vipindi mbalimbali vinavyoitwa awamu. Utekelezaji wa miradi mingi kwa utaratibu wa awamu nyingi za

utekelezaji umesababisha gharama isiyoendana na thamani halisi ya fedha zinazotumika. Kwa mfano mradi wa Matengenezo ya Barabara ya Nakwa iliyopo Mkoa wa Manyara yenye urefu wa kilometa 9, kwa Kiwango cha lami ambao umepangwa kutekelezwa katika awamu zaidi ya tano (5); katika awamu hii unajengwa kwa urefu wa KM 0.7. Hali hiyo inachelewesha upatikanaji wa manufaa ya mradi huo kiuchumi na kijamii kwa umma.

**(b) Ujenzi wa Majengo Usioendana na Uhaba wa Ardhi**

**Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa mambo ya msingi katika miradi ya ujenzi wa majengo ya umma ni uzingatiaji wa matumizi bora ya ardhi iliyopo. Katika ukaguzi wa miradi inayotekelezwa, Kamati ilibaini kuwa ipo baadhi ya miradi ya ujenzi inayotekelezwa bila kuzingatia uhaba wa ardhi. Kwa mfano, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD), Ujenzi wa Jengo la X-Ray, Ujenzi wa Jengo la Maabara na Ujenzi wa Jengo la Kuhifadhia Maiti katika Hospitali ya Wilaya ya Arusha umeanza na kuendelea kuwa na majengo ya chini ingawa eneo la ardhi ya Hospitali hiyo haliwezi kuongezeka sambamba na ongezeko la mahitaji kwa siku zijazo.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii itasababisha ugumu wa utekelezaji wa miradi siku zijazo kutokana na uwezekano wa kukosekana kwa ardhi.

**(c) Changamoto ya Mfumo wa Ulipaji**

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo hufanyika sambama na malipo yanayostahili. Kwa Upande wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Malipo hufanyika kwa kutumia **Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE).** Katika baadhi ya miradi imebainika kuwa kuna

wakati malipo yaliyostahili yalikwama kutokana na changamoto za MUSE kutoweza kutumika kufanya malipo kwa muda mrefu, jambo lililochelewesha utekelezaji wa mradi. Mfano wa mradi uliokwama kutokana na changamoto hiyo ni Ujenzi wa Jengo la OPD, Ujenzi wa Kichomea Taka, Ujenzi wa Jengo la Maabara na Ukarabati wa majengo ya katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Hali hiyo inaathiri gharama na kuchelewesha utekelezaji wa miradi.

**Mheshimiwa Spika**, Ufafanuzi zaidi wa hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo unapatikana katika Kiambatisho cha taarifa hii. Kamati ina maoni kuwa, mambo hayo yanayoathiri tija inayokusudiwa kwenye miradi yanahitaji kutatuliwa kwa mwaka huu na kuwa mazingatio kwa miradi mipya.

### 2.1.2 Hatua za Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwenye Kamati ulifanyika sambamba na kujiridhisha iwapo ushauri uliotolewa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ulizingatiwa. Lengo ni kutafakari utoaji wa maoni na ushauri kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kulingana na uzingatiaji wa maoni na ushauri kwa mwaka uliopita.

**Mheshimwa Spika,** wakati wa Kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rasi TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2023/2024, tarehe 14 Aprili, 2023, Kamati ilitoa maoni na kushauri katika maeneo kumi na sita ya utekelezaji wa Bajeti hii.[1] Kwa madhumuni ya kujiridhisha na uzingatiaji wa maoni na ushauri

[1] Tazama, Taarifa Rasmi za Bunge, Majadiliano ya Bunge ya Tarehe 14 Aprili, 2023.

huo, tarehe 18 - 26 Machi, 2024 Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu uzingatiaji wa maoni na ushauri huo.

**Mheshimiwa Spika,** Maelezo yaliyowasilishwa yalionesha kwamba, Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati. Uchambuzi wa maelezo hayo umedhihirisha kuwa, sehemu kubwa ya ushauri imefanyiwa kazi, sehemu nyingine inaendelea kuzingatiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya maeneo 16 yaliyotolewa ushauri, yapo maeneo yaliyozingatiwa ipasavyo na mengine kwa kiwango kisichokamilika. Aidha, yapo maeneo ambayo hayajazingatiwa kabisa. Mfano wa ushauri uliozingatiwa kikamilifu ni kuhusu uanzishaji wa mifumo itakayowezesha uagizaji wa vitendanishi, vifaa tiba na dawa kupitia MSD. Kamati ilishauri kuwa Serikali iweke mifumo hiyo ili kufikia malengo ya Serikali ya kufikisha huduma kwa wananchi kwa haraka na kwa ubora zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** maelezo ya Waziri yalionyesha kuwa TAMISEMI imeweka mfumo maalum ujulikanao kama *Redisigned Integrated Logistic Management Information System (RILS)*. Hatua hiyo inatokana na usikivu wa Serikali kwa Kamati. Aidha, TAMISEMI imeahidi kuendelea kuimarisha matumizi ya Mfumo huo uliowezesha vituo vya kutoa huduma za afya kupokea bidhaa ndani ya siku 21 baada ya kuagiza tofauti na awali vilipokuwa vikitumia siku 60 hadi 90.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa ushauri ambao uzingatiaji wake unaendelea ni kuhusu utoaji wa mafunzo ya awali *(Induction)* kwa Watendaji wa Kata na Watendji wa Vijiji. Kamati ilishauri kuwa Ofisi ya Rais TAMISEMI iratibu mafunzo ya awali kwa Watendaji wa Kata na Vijiji ili kuongeza uwajibikaji katika ngazi za vijiji na kata. Taarifa ya Serikali ilionyesha kuwa mafunzo hayo yaliendeshwa

kwa Watendaji wa Kata 1,758 kati ya 3956 walioajiriwa. Ushauri huu umeanza kutekelezwa lakini utaendelea kwa mikoa ambayo bado na kwa Watendaji wa Vijiji *(VEO)*.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi za Ofisi ya Rais TAMISEMI kuzingatia ushauri uliotolewa, bado haijafanikisha utekelezaji wa maeneo machache yaliyotolewa ushauri. Kwa mfano, Kamati ilishauri kuwa Serikali ipeleke fedha za kumalizia maboma ya shule, vituo vya afya na zahanati yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi ili kuondoa hasara inayoweza kupatikana kutokana na kuchakaa kwa majengo haya. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI alieleza kuwa Serikali imefanya zoezi la tathmini za viporo vya maboma hayo. Maelezo hayo ni ishara kuwa fedha hizo hazijapelekwa na kwamba hazijatengwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

### 2.1.3 Hatua zilizofikiwa katika Utekelezaji wa Bajeti

#### (a) Hali ya Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

**Mheshimiwa Spika**, ukusanyaji wa mapato ni sehemu ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Kamati ilizingatia hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, aliyoitoa Bungeni tarehe 14 Aprili, 2023 akiwasilisha Makadirio ya Ofisi hiyo kwa ajili ya kupitishwa na Bunge. Katika Hotuba hiyo, jumla ya **Sh. Trioni 1.19** zililengwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Ili kulisaidia Bunge kufuatilia utekelezaji wa jambo lililoelezwa, Kamati ililinganisha makusanyo halisi na lengo lililokuwa limebainishwa.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulijulisha Bunge tathmini ya hali ya ukusanyaji wa mapato iliyobainika. Kwa ujumla, matokeo ya uchambuzi yameonesha kama ifuatavyo:-

(i) Jumla ya kiasi cha fedha zilizokusanywa hadi kufikia Mwezi Februari, 2024 ni sh. Bilioni 756.48 sawa na asilimia 63.8 ya lengo. Mwenendo huo unaashiria uwezekano wa kufikiwa kwa lengo, jambo ambalo linaonesha ufanisi na upangaji unaozingatia hali halisi; na

(ii) Uwiano wa mchango wa makusanyo ya maduhuli kutoka Makao makuu ya Wizara na Taasisi zake ikilinganishwa na mchango wa mikoa 26 na halmashauri 184 nchini unatofautiana na uwiano halisi wa makusanyo. Uwiano wakati wa makadirio ulikuwa ni asilimia 4 kwa asilimia 96 za mchango wa wizara na taasisi zake na mikoa na halmashauri zote mtawalia. Uwiano wa hali halisi umekuwa asilimia 2 kwa asilimia 98 mtawalia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa matokeo hayo ni dhahiri kuwa: -

i) Kuna uwezekano mkubwa wa lengo la maduhuli kuwa limetokana na hali halisi, kwa sababu hakuna tofauti ya uwiano; na

ii) Kuna uwezekano mkubwa wa makusanyo halisi kuzidi kidogo lengo lililowekwa, kwa kuwa makusanyo makubwa yalipatikana kabla ya kufikia mwisho wa robo ya tatu ambayo ni mwisho wa mwezi Machi, 2024.

**(b) Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge imeweka sharti la kufanya uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa kulinganisha na hali halisi ya mwaka unaotangulia. Kamati ilichambua kwa mtazamo huo na kubaini yafuatayo:-

(i) Jumla ya fedha iliyopokelewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI hadi kufikia mwezi Februari, 2024 ni sawa na asilimia 68.06 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kwa mwenendo huo, kuna uwezekano wa Ofisi ya Rais TAMISEMI kupata kiasi chote cha bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Ikiwa hivyo, majukumu na mipango yote iliyopangwa ina mwelekeo wa kukamilishwa;

(ii) Uwiano wa Bajeti ulioidhinishwa na Bunge tarehe 18 Aprili, 2023 ulionesha kuwa Makao Mkauu ya Wizara na Taasisi zake pamoja na Tume ya Utumishi wa Walimu ingepata aslimia 12.32 ya Bajeti ya Ofisi hii, na Mikoa 26 Tanzania Bara na Halmashauri 184 ingepata asilimia 86.68 ya Bajeti ya TAMISEMI. Hali halisi ya upatikanaji wa fedha imebainisha uwiano tofauti na uliopitishwa na Bunge. Makao Makuu ya Wizara na Taasisi zake pamoja na Tume ya Utumishi wa Walimu imepokea aslimia 15.1 ya fedha yote iliyopokewa, na Sekretarieti za Mikoa 26 pamoja na Halmashauri 184 zimepokea asilimia 84.9 ya fedha zilizopokewa na TAMISEMI;

(iii) Uwiano wa Bajeti ya Maendeleo kwa bajeti ya matumizi ya kawaida wakati Bunge lilipopitisha makadirio ni tofauti kidogo na uwiano wakati wa utekelezaji. Bunge lilipopitisha Bajeti ya Wizara hii uwiano ulikuwa ni asilimia 33.3 kwa asilimia 66.7 mtawalia. Uwiano wa fedha zilizopatikana kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa kiasi cha fedha zilizopatikana kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni asilimia 38.03 kwa asilimia 61.07 mtawalia; na

(iv) Uwiano wa Bajeti ya Maendeleo kwa Makao Makuu ya Wizara na taasisi zake ukilinganishwa na bajeti ya maendeleo kwa mikoa na halmashauri zote nchini

unatofautiana na uwiano halisi wa kiasi cha fedha kutoka hazina kwa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na taasisi hizo. Wakati uwiano wa bajeti ya maendeleo iliyopitishwa na Bunge kati ya TAMISEMI na taasisi zake kwa upande mmoja na Seketarieti za mikoa na halmashauri zote kwa upande mwingine ni asilimia 29 kwa asilimia 71 mtawalia. Lakini upokeaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa taasisi hizo ni asilimia 36.8 kwa 63.1 mtawalia.

**Mheshimiwa Spika** kwa mwenendo huo, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya majukumu ya OR - TAMISEMI Makao Makuu na Taasisi zake ni mzuri zaidi ya upatikanaji wa fedha kwa Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri nchini. Ilhali Makao Makuu ni Waratibu na Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri ni Watekelezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilirejea majadiliano ya Wizara na Kamati ya tarehe 18 hadi 26 Machi, 2024 na kubaini yafuatayo:-

(i) Fedha zilizopokewa Makao Makuu ya Wizara ni kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya kusimamia na kuratibu uendeshaji wa shughuli za Sekretarieti za Mikoa 26 Tanzania Bara, Tume ya Utumishi wa Walimu na uendeshaji wa Makao Makuu ya Wizara.

(ii) Fedha zilizopokewa kwenye Sekretarieti za Mikoa 26 ya Tanzania Bara ni kwa ajili ya shughuli za umma kwenye Wilaya 139, Tarafa 570, Halmashauri 184, Kata 3,956, Vijiji 12,318, Mitaa 4,263 na Vitongoji 64,361.

(iii) Fedha zilizopokewa na Tume ya Utumishi wa Walimu ni kwa ajili ya kufanikisha dhima ya Tume hiyo ya kuhakikisha walimu wa shule za msingi na sekondari wanapata huduma bora

kuhusu masuala ya ajira, kupandishwa vyeo na kukuza maadili.

**(c) Hali ya Utekelezaji wa Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa mpango wa Wizara au taasisi yoyote kwa mwaka wa fedha unaoisha, ni kigezo muhimu cha kupanga kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa kuzingatia msingi huo, kabla ya kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi, Kamati ilichambua hali ya utekelezaji wa mpango wa Ofisi ya Rais, TIMISEMI kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Katika uchambuzi huo miongoni mwa mipango ilihusu ukamilishaji wa Sera ya Taifa ya Ugatuaji, Program ya Kuimarisha Mikoa na Serikali za Mitaa na usanifu wa mifumo ya TEHAMA katika ngazi zote za OR – TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa mambo hayo yanaendelea kutekelezwa. Kwa mfano, usanifu wa mifumo ya TEHAMA na uendeshaji wa tovuti 211 za OR – TAMISEMI ni mambo endelevu. Hata hivyo, utekelezaji ulipaswa kuzingatia uhusiano na ushirikiano kati ya OR – TAMISEMI na taasisi zake katika suala la usimamizi wa tovuti za taasisi hizo. Kwa mfano usimamizi wa tovuti ya Chuo cha Serikali za Mitaa ulistahili kuonekana wazi wazi katika ripoti ya utekelezaji. Aidha, maandalizi ya ukamilishaji wa Sera ya Taifa ya Ugatuaji ni jambo linalostahili kupewa uzito maalum.

## 2.2 Uchambuzi wa Mpango kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa makadirio ya Mapato na matumizi unazingatia mipango ya Wizara na Taaasisi inayohusika. Ili kukidhi

mantiki ya Bunge kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilichambua mipango ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI na kubaini yafuatayo: -

(i) Mipango ya OR - TAMISEMI inatekelezwa kwa kigezo cha vipaumbele 12 vilivyochaguliwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na ugatuaji wa madaraka kwa umma (D by D) ni kipaumbele cha kwanza. Hata hivyo, kipaumbele hiki kimeamuliwa bila ya kuwa na Sera ya Taifa ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma iliyokamilika;

(iii) Kusimamia mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato ni kipaumbele kinachoendana na mahitaji kulingana na yaliyobainika wakati wa ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kamati ilipotembelea miradi ya maendeleo ilibaini kuwa kitengo cha ufuatiliaji na uratibu kina ufanisi mdogo katika kuratibu miradi inayotekelezwa kwenye mikoa na halmashauri mbalimbali nchini;

(iv) Kwa ujumla mipango hiyo inahusiana moja kwa moja na majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI yaliyoainishwa katika Hati Idhini ya kuanzishwa kwake;

(v) Baadhi ya Mipango iliyotekelezwa mwaka wa fedha 2023/2024 haikujitokeza waziwazi katika mipango inayokusudiwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(vi) Baadhi ya Mipango iliyotekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 imeendelea kujitokeza kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na

(vii) Baadhi ya mipango inayojitokeza kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni mipya na haikuwepo katika mwaka wa fedha 2023/2024.

## 2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, tija na manufaa ya mipango yoyote ya kuboresha shughuli za umma, vinategemea kwa kiasi kikubwa makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali. Ili kujiridhisha na uwezekano wa manufaa kwa umma yanayoweza kupatikana kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati imechambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Uchambuzi huo umehusisha kutathmini mambo makuu matatu ambayo ni: Makadirio ya Mapato, makadirio ya matumizi ya kawaida na makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo. Ufafanuzi wa matokeo ya Uchambuzi ni kama ifuatavyo:-

### 2.3.1 Uchambuzi wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia uhusiano uliopo kati ya uendeshaji wa shughuli za umma, ukusanyaji wa maduhuli na uwiano wa mapato kwa matumizi. Kwa msingi huo uchambuzi ulifanyika kwa kulinganisha na makadrio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha ulioisha, hali halisi ya ukusanyaji wa maduhuli hadi kufikia mwezi Februari, 2024 na lengo la Serikali kuhusu ukusanyaji. Matokeo ya uchambuzi yameonyesha kama ifuatavyo: -

i) Makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yameongezeka kwa asilimia 14 ikilinganishwa na makadirio kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

ii) Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024 unaonesha uwezekano wa kufanikisha

ongezeko la lengo la makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2024/2025;

iii) Uwiano wa makadirio ya maduhuli kwa makadirio ya bajeti ya matumizi kwa OR - TAMISEMI kwa mwaka 2023/2024 ulikuwa ni asilimia 13.05 ya bajeti ya makadirio ya matumizi. Uwiano wa mkadirio ya maduhuli kwa bajeti ya matumizi umekuwa asilimia 13.46 ya bajeti ya matumizi kwa mwaka 2024/2025.

### 2.3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, uendeshaji wa shughuli za umma hutegemea bajeti ya matumizi ya kawaida. Aidha, mahitaji ya kibajeti ya shughuli za uratibu hayalingani na mahitaji ya shughuli za utekelezaji. Kwa misingi hiyo Kamati ilichambua ili kujiridhisha na tofauti zinazotakiwa. Uchambuzi umebanisha yafuatayo: -

i) Bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa asilimia 19.4 ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

ii) Matumizi ya kawaida ya OR - TAMISEMI na taasisi zake yameongezeka kwa asilimia 9 wakati bajeti ya matumizi ya kawaida *(recurrent)* kwa Sekretarieti za Mikoa 26 na Halmashauri 184 imeongezeka kwa asilima 19.6; na

iii) Ongezeko la bajeti ya matumizi ya kawaida linaendana na nyongeza ya vipaumbele vya mpango wa bajeti ya OR - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

### 2.3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa miradi ya maendeleo unatarajiwa kusaidia huduma kwa umma kwa muda mrefu.

Utekelezaji huo unategemea bajeti inayopitishwa na Bunge. Aidha, OR - TAMISEMI na taasisi zake zinatekeleza baadhi ya miradi pamoja na kusimamia utekelezaji wa miradi katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uchambuzi wa bajeti ya miradi ya maendeleo umebainisha mambo yafuatayo: -

i) Kwa ujumla bajeti ya miradi ya maendeleo imepungua kwa asilimia 2 kwa mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

ii) Bajeti ya mandeleo kwa Makao Makuu ya OR - TAMISEMI na taasisi zake imeongezeka kwa asilimia 2;

iii) Bajeti ya miradi ya maendeleo kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa imepungua kwa asilimia 3.7.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo chini ya OR - TAMISEMI yameongezeka kutokana na hali halisi ya baadhi ya miradi. Kamati imeridhishwa na makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo. Kamati ina maoni kwamba wakati wa utekelezaji wa bajeti hii Serikali itapaswa kuzingatia ushauri unaotolewa na Wabunge pamoja na ushauri wa Kamati.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** lengo la uchambuzi uliowekewa utaratibu na kanuni za kudumu za Bunge ni kuwezesha upatikanaji wa maoni na ushauri. Naomba kulishauri Bunge lako Tukufu lijadili makadirio ya mapato na matumizi ya OR - TAMISEMI kwa pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kama unavyofafanuliwa katika taarifa hii.

### 3.2 Maoni na Ushauri

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na matokeo ya uchambuzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha zilizoidhiniswha na Bunge na vipaumbele vilivyobainishwa na OR - TAMISEMI, Kamati inashauri kuhusu mambo mbalimbali ya kuzingatiwa wakati wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, baada ya uchambuzi wa makadirio wa mapato na matumizi ya OR - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Kamati inashauri kama ifuatavyo: -

#### 3.2.1 Umaliziaji wa Maboma ya Shule na Zahanati

**Mheshimiwa Spika**, katika kufanikisha ujenzi wa majengo mbalimbali nchini wananchi wamejitolea kujenga majengo mengi kwa ajili ya shule na zahanati kwa ajili ya huduma kwa umma. Ujenzi huo uliofanyika kwa nguvu za wananchi umefikia hatua ya upauaji lakini haujaendelezwa. Kwa sababu hiyo, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

i. Serikali itekeleze ushauri wa Kamati ulitolewa wakati wa uwasilishaji wa maoni ya Kamati kuhusu bajeti ya OR - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

ii. Serikali itoe mwongozo na kuweka uratibu stahili katika uanzishwaji wa ujenzi wa majengo ya aina hiyo kwa nguvu za wananchi ili kupunguza ujenzi holela wa maboma na kudhibiti viwango vya ujenzi wa maboma ya majengo ya Serikali; na

iii. Serikali kuzingatia ombi maalum la kibajeti lililowasilishwa na Kamati kuhusu umaliziaji wa maboma hayo.

### 3.2.2 Fedha kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu iliyoharibiwa na mvua nchini;

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2023/2024 Serikali ilitenga zaidi ya shilingi trilioni moja kwa ajili ya TARURA. Hata hivyo, upelekaji wa fedha hizo ulifikia asilimia 45.7 Upokeaji huu hauridhishi na hautaiwezesha TARURA kutekeleza miradi yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia mwishoni mwa mwaka 2023 hadi sasa nchi imekumbwa na uharibifu mkubwa wa miundombinu ya Barabara katika maeneo mbalimbali nchini kutokana na kunyesha kwa mvua kubwa za El Nino. Hali hii imesababisha Barabara nyingi hasa za vijijini kutokupitika kabisa kutokana na uharibifu huo na hivyo kusababisha huduma mbalimbali za usafiri kwa wananchi kuwa ngumu. Kutokana na hali hiyo OR - TAMISEMI imeweka mkakati wa kuzirejesha Barabara hizo katika hali yake ya kawaida kwa kuitumia TARURA.

**Mheshimiwa Spika,** azma ya OR - TAMISEMI kusimamia miradi ya ujenzi wa barabara na miundombinu inayoendana na barabara hizo inaweza kufanikiwa kwa kuongeza fedha kwa Wakala wa Baraba Vijijini na Mijini (TARURA). Hivyo, Kamati

inashauri Serikali kuzingatia ushauri wa Kamati uliotolewa katika Bunge la Bajeti lililopita, pamoja na hayo, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo: -

i. Kupeleka fedha TARURA kikamilifu na kwa wakati; na

ii. Kutoa bajeti ya dharura kwa kuzingatia ombi maalum lililotolewa na Kamati kwa ajili ya kusaidia urejeshaji wa miundombinu hiyo.

### 3.2.3 Ushiriki wa wakandarasi wazawa katika utekelezaji wa miradi

**Mheshimiwa Spika**, katika orodha ya vipaumbele vya OR - TAMISEMI ushirikishwaji wa wananchi ni jambo lililopewa uzito. Aidha, OR - TAMISEMI imepanga kuratibu na kusimamia miradi ya ujenzi katika ngazi zote za Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa.

**Mheshimiwa Spika,** Katika vikao vyake na OR - TAMISEMI Kamati ilibaini kuwa Serikali imekuwa ikitumia zaidi wakandarasi ambao si wazawa na hivyo kuwanyima wakandarasi wazawa fursa ya utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha, wakandarasi wengi wazawa huwa na mitaji midogo ambayo inaonekana kutokutosheleza utekelezaji wa miradi inayoratibiwa na Serikali kutokana na ugumu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo Kamati inashauri kuwa kipaumbele cha kutoa kandarasi kwa wakandarasi wazawa kizingatiwe sambamba na kuzielekeza halmashauri nchini kuwatumia wakandarasi wazawa lakini bila kuathiri viwango stahifu.

### 3.2.4 Uanzishwaji na uendeshwaji wa shule za msingi za michepuo wa Kiingereza

**Mheshimiwa Spika**, katika mpango wa OR - TAMISEMI unaohusu kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma za jamii yapo mambo ya msingi yanayopaswa kuzingatiwa. Msimamo wa Serikali kuhusu huduma hizo ni jambo la lazima. Katika uchambuzi wa Randama za OR - TAMISEMI Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa maoni ya Kamati kuhusu uanzishwaji wa shule za mchepuo wa Kiingereza yaliyotolewa katika taarifa yake wakati Bunge linapitisha bajeti ya OR - TAMISEMI (tarehe 14 – 18 Aprili, 2023) hayakueleweka. Kwa ujumla Kamati inaona kuwa kuanzishwa kwa shule hizi utaleta matabaka kwa Watanzania na pia kwenda kinyume na Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 Toleo la 2023.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo Kamati inashauri kuwa, Serikali izingatie ushauri wa Kamati juu ya utoaji wa elmu kwa kuzingatia usawa na kuimarisha ufundishaji wa somo la kiingereza katika shule zake zote.

### 3.2.5 Utekelezaji wa wajibu wa Wadau wa Miradi ya Mendeleo kurudisha faida kwa Jamii (CSR)

**Mhesimiwa Spika**, katika uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024 Kamati ilibaini kuwa OR - TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikipata fedha kutoka kwa watekelezaji wa miradi mbalimbali kama sehemu ya uwajibikaji wa taasisi na kampuni zinazotekeleza miradi hiyo kwa jamii *(Corporate Social Responsibility – CSR)*. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa miongozo ya matumizi ya fedha hizo bado haileti tija inayotarajiwa kwa wananchi. Aidha, Kamati imebaini kuwa

hakuna miongozo kwa halmashauri ya namna ya kuwatambua wadau wanaotekeleza miradi ya maendeleo kwa kuwa kuna miradi mingi inayotekelezwa na wadau mbalimbali wa maendeleo bila wadau hao kupata fursa ya kurejesha faida kwa jamii. Kamati pia imebaini kuwa katika baadhi ya maeneo wadau hao wamekuwa wakiratibu na kutekeleza miradi hiyo wenyewe bila usimamizi na uratibu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hiyo Kamati inashauri kuwa utekelezaji wa miradi uende sambamba na kusimamia utaratibu wa wajibu wa wadau wa miradi hiyo kurejesha faida kwa jamii. Kutokana na hilo Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

i. Utekelezaji wa miradi hiyo ulizingatie sheria, miongozo na kanuni ya utekelezaji wa miradi ya Serikali;

ii. Usimamizi wa gharama za miradi ya fedha zinazotokana na CSR ufanywe kwa kufuata kanuni na taratibu za manunuzi za Serikali ili kuepuka gharama kubwa za miradi hiyo; na

iii. Halmashauri zibainishe taasisi zote za kibiashara katika maeneo yao ambazo zinapaswa kutoa CSR na kuhakikisha kuwa taasisi hizo zinarejesha faida kwa jamii.

### 3.2.6 Mapato ya Halmashauri kutokana na biashara ya Kaboni

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mpango wa OR - TAMISEMI wa kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato, halmashauri zimekuwa zikibuni vyanzo mbalimbali vya mapato. Katika vikao vya kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya OR - TAMISEMI Kamati ilibaini kuwa kuna chanzo cha biashara ya kaboni kinachoziingizia mapato ya kutosha halmashauri chache nchini ambacho hakijagunduliwa na

halmashauri nyingine. Kutokana na hilo Kamati inashauri kama ifuatavyo: -

i. Serikali ihakikishe kuwa eneo la biasahara ya Kaboni lipewe kipaumbele kama chanzo muhimu cha mapato ya halmashauri zote zilizo na utajiri wa misitu nchini;

ii. OR - TAMISEMI ijenge uwezo wa kitengo kinachosimamia biashara ya kaboni ili kuweza kutoa ushauri wa kitaalam kwa halmashauri nchini; na

iii. Serikali za vijiji, kata na halmashauri zipime maeneo na kumilikishwa maeneo hayo kama hatua ya kuweza kuhifadhi na kuitunza misitu wenyewe ili iweze kuwanufaisha katika biashara ya kaboni.

### 3.2.7 Utunzaji wa Mazingira katika Halmashauri

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato ni sehemu ya lengo la OR - TAMISEMI, uboreshaji wa mazingira ni sehemu muhimu katika kuziwezesha halmashauri kujiongezea kipato kutokana na mazingira kuweza kuwa kama chazo cha mapato kwa ajili ya biashara ya Kaboni. Kutokana na hiyo Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

i) Serikali ianzishe programu maalumu katika shule za msingi na sekondari nchini kwa kila mwanafunzi anayeanza shule kupanda na kuutunza mti wake wakati wa maisha yake yote awapo shuleni hapo;

ii) Mashirika yanayotoa misaada ya kupanda miti yaelekezwe kujikita kwenye ujenzi wa miundombinu ya kutunzia miti; na

iii) Halmashauri nchini zielekezwe kuweka sheria ndogo *(by laws)* kwa ajili ya kusimamia wajibu wa wananchi kupanda miti na kuitunza kwenye maeneo ya makazi yao;

### 3.2.8 Uhuishaji wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali, Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Sheria ya Manunuzi ya Umma

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali, Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Sheria ya Manunuzi ya Umma zimeweka masharti ambayo ni ngumu kutekelezeka katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa mfano upatikanaji wa mashine za EFD kwa huduma kama za mazishi au vyakula zinazotolewa maeneo ya vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa malengo ya OR - TAMISEMI kwa mwaka 2024/2025 ni kuratibu utoaji wa huduma kwa jamii. Kamati imebaini kuwa hoja nyingi za ukaguzi za CAG zinatokana na sheria hizo kuleta changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ngazi ya kata, vijiji na halmashauri.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika uchambuzi wake ilibaini kuwa pamoja na utoaji huduma kwa jamii kwa kipindi cha mwaka 2023/2024 kuwa na mafanikio pia imebainika utekelezaji wa shughuli za Serikali za Mitaa umekuwa ukiathiriwa na zilizotajwa hapo juu. Kutokana na ugumu wa utekelezaji kwa kufuata sheria hizo imebainika kuwa halmashauri zimekuwa zikikutana na hoja nyingi za kihasibu kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

**Mheshimiwa Spika,** ili utekelezaji wa bajeti inayoombwa na OR - TAMISEMI izingatie uhalisia katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Kamati inashauri kuwa, Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Umma pamoja na Sheria ya Manunuzi ya Umma zinahitaji kuhuishwa ili ziendane na mazingira halisi ya utekelezaji wa shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### 3.2.9 Taasisi za Serikali zinazofanya kazi na Halmashauri kuzingatia bajeti za Halmashauri

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya OR - TAMISEMI kwa mwaka 2023/2024 katika utekelezaji wa bajeti za halmashauri Kamati ilibaini kuwa zipo taasisi zinazoandaa makongamano, warsha na semina mbalimbali na kuwaalika wataalam wa halmashauri huku zikiwaelekeza wakurugenzi wa halmasahuri hizo kugharamia. Hali hii imekuwa ikizifanya halmashauri hizo kutumia fedha ambazo hapo awali hazikuwa kwenye bajeti yao, na hivyo kufanya shughuli nyingine za kibajeti katika halmasahuri hizo kutokutekelezwa. Kamati inashauri OR - TAMISEMI kuelekeza kuwa mialiko yoyote itakayokwenda kwa wakurugenzi iambatane na taarifa ya walioandaa matukio hayo kuonesha kuwajibika kwao kibajeti.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa kunipatia fursa ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu. Nawashukuru sana Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengewa (Mb), – Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Waheshimiwa Naibu Mawaziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Festo John Dugange pamoja na Mheshimiwa Zainab Katimba kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Wizara ya TAMISEMI, Ndg. Adolf H. Ndunguru pamoja na Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati tangu tulipoanza kufanya nao kazi na kushiriki vizuri kwenye uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee namshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga (Mb), pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja, kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa. Wajumbe hawa ni wachapa kazi na wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa Bajeti na kuhakikisha wanahoji ili kupata ufafanuzi wa kina.  Nawapongeza sana na naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Lazaro Justin Nyamoga, Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
2. Mhe. William Vagimembe Lukuvi, Mb.
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb.
4. Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi, Mb.
5. Mhe. Sylvestry Fransis Koka, Mb.
6. Mhe. Zuberi Mohammed Kuchauka, Mb.
7. Mhe. Zacharial Paulo Issaay, Mb.
8. Mhe. Salome Wycliff Makamba, Mb.
9. Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara, Mb.
10. Mhe. Sebastian Simoni Kapufi, Mb.
11. Mhe. Amandus Julius Chingulile, Mb.
12. Mhe. Dorothy George Kilave, Mb.
13. Mhe. Elinikyo Mafuwe Saashisha, Mb.
14. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb.
15. Mhe. Mwantum Mzamili Zodo, Mb.
16. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis, Mb.
17. Mhe. Erick James Shigongo, Mb.
18. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb
19. Mhe. Ameir Abdalla Ameir, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema, katika wakati wote ilipokutana ikiwemo Taarifa hii.

### 4.2 Mwisho

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zake (**Fungu 56, 02, 36 ,47, 54, 63, 70, 71, 72, 79, 74, 75, 76, 77, 78, 79, 80, 81, 82, 83, 84, 85, 86, 87, 88, 89, 90, na 95)** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja, jumla ya **Shilingi 10,163,499,893,167.00.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumaliza, kwa niaba ya Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ninaunga mkono Hoja.

**Mheshimiwa Spika** Naomba Kuwasilisha.

Dennis Lazaro Londo, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

16 APRILI, 2024

***JEDWALI NA. 1:* TAARIFA YA MIRADI ILIYOKAGULIWA NA KAMATI KWA KIPINDI CHA MWEZI MACHI, 2024**

| NA. | JINA LA MRADI | MAHALI ULIPO | HALI YA UTEKELEZAJI WA MRADI | CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA WAKATI WA UTEKELEZAJI WA MRADI | MAONI YA KAMATI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Manyara | Babati Mjini | hadi Kamati ilipotembelea mradi huu ulifikia asilimia zaidi ya 65 na kutumia kiasi cha shilingi 1,734,538,386 zimekwishakutumika | a) Kutokupatikana kwa mafundi kwa wakati;<br>b) Udogo wa eneo umesababisha kujenga majengo katika pande zote mbili zilizotengwa;<br>c) Baadhi ya wazabuni kuhitaji malipo kabla ya kuleta bidhaa *(Pre-payment)* kinyume na taratibu za manunuzi ya umma zilizopo; | a) Kamati imefurahishwa na ushirikiano wa Serikali na taasisi zake Mkoani Manyara. Kamati inashauri Mikoa mingine yote kufanya kazi kwa umoja na ushirkiano wa karibu;<br>b) Kamati inashauri Miradi inayotekelezwa katika Halmashauri kutumia wakandarasi wazawa ili kuongeza uzalendo lakini;<br>c) Seikali isimamie upatikanaji wa ujenzi wa miradi mbalimbali, hasa shule na zahanati ilikuondoa uwezekano wa miradi kupelekwa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | d) Uhaba wa baadhi ya bidhaa za ujenzi;<br><br>e) Eneo la ujenzi kukosa miundombinu muhimu kama Barabara, maji na umeme. | maeneo ambayo hayastahili kujengwa mirahi husika. |
| 2. | Mradi wa Matengenezo ya Barabara ya Nakwa kwa Kiwango cha Lami (KM 0.7) – Mkoa Wa Manyara (Mradi Namba 4170 - AE/092/2022/ 2023/MNR/W/ 17) | Babati Mjini | Kamati inatembelea mradi huu utekelezaji ulifikia asilimia 100 kwa kipande kilichopang wa kutekelezwa katika kipindi cha 2023/2024 | ufinyu wa bajeti, hali inayosababisha barabara hii yenye urefu wa Km 9 kujengwa kwa awamu nyingi. | Serikali iwe inatenga bajeti kamili inayotosha kukamilisha Barabara inayopangwa ili Barabara iishe kwa wakati ili iweze kuleta thamani ya fedha inayowekwa na huduma inayotarajiwa |
| 3. | Mradi wa Matengenezo ya Barabara | Halmashau ri ya Wilaya | hadi wakati Kamati inatembelea | Kunyesha mvua zilizo juu ya wastani zilipelekea | Serikali iwe inatenga bajeti kamili inayotosha kukamilisha |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | ya Nakwa kwa Kiwango cha Lami (KM 0.7) – Mkoa Wa Manyara (Mradi Namba 4170 -AE/092/2022/ 2023/MNR/W/ 17) | ya Hanang' | mradi huu (mwezi March, 2024) utekelezaji mradi ulifikia hatua ya kuandaa | kuporomoka /kumomonyoka kwa ukingo wa Barabara, hali iliyosababisha kufanyika mabadiliko ya kimkataba kukabili madhara hayo. | Barabara inayopangwa ili Barabara iishe kwa wakati |
| 4. | Mradi wa Matengenezo ya Barabara ya RHM-Oltrumet Hospital kwa kiwango cha lami Ngumu (0.5km) (Mradi Namba 4170 -(S10/001/2023 /2024/W/43) | Halmashauri ya Wilaya ya Arusha | Hadi wakati Kamati inatembelea na mradi huo, ulikuwa umetekelezwa kwa asilimia zaidi ya 80 | Mvua zilizo juu ya wastani zilipelekea kuporomoka/kumomonyoka kwa ukingo wa Barabara. Imesababisha kufanya mabadiliko ya kimkataba kukabili madhara hayo. | ➢ Kwa hizi Barabara zenye urefu wa chini ya kilometa 10 Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti inayoweza kutosha ujenzi wa Barabara nzima;<br>➢ Serikali itoe motisha kwa wananchi ambao wamejitolea maeneo yao kutumika kwa ajili za mchepuko ili kuwaongezea hamasa ya uzalengo wananchi. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 5. | Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Longido Sekondari-Kanisa Katoliki kwa Kiwango cha Lami Mita (0.5 Km) Mradi Namba 4170 (S10/001/2023 /2024/W/69) | Halmashauri ya Wilaya ya Longido | Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu (mwezi March, 2024) ulifikia asilmia zaidi ya 75 | Utekelezaji wa mradi huu umekumbwa na changamoto ya kunyesha mvua zilizo juu ya wastani ilipelekea kuporomoka /kumomonyoka kwa ukingo wa Barabara. | i. Serikali ihakikishe kuwa inawasimamia wakandarasi ili waweze kutekeleza kuomba fedha kama ilivyopangwa ili kutoruhusu fedha za miradi mingine kutumika pasipo kupangwa.<br>ii. Serikali ichukue ujenzi wa Barabara hii kama mfano wa kujenga Barabara nyingine zote katika halmashauri mbalimbali nchini. |
| 6. | Mradi wa Ujenzi wa Jengo la OPD, Ujenzi wa Jengo la X-Ray, Ujenzi wa Jengo la Maabara, na | Halmashauri ya Wiilaya ya Arusha | Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu ulikuwa uko kwenye hatua za msingi | - | i. Serikali iweke mkakati wa kuanza kujenga majengo ya ghorofa katika miradi ya hospitali na |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Ujenzi wa Jengo la Kuhifadhia Maiti katika Hospitali ya Wilaya ya Arusha – Mradi Namba: 6212 | | | | ii. Serikali itenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika eneo lote linalozunguka hospitali; |
| 7. | Mradi wa Ujenzi wa Jengo la OPD, Ujenzi wa Kichomea Taka cha Kisasa, Ujenzi wa Jengo la Maabara na Ukarabati wa Majengo ya Hospitali Katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Meru (Mradi Namba 6212) | Wilaya ya Arumeru | Hadi Kamati inatembelea mradi huu ulikuwa umefikia zaidi ya asilimia 50 | Matumizi ya Mfumo wa MUSE na FFARS, ambapo mifumo hii imekuwa ikisumbua wakati wa mapokezi ya fedha na kusababisha mradi kuchelewa kuanza.<br><br>Kupanda kwa bei za vifaa vya ujenzi na uadimu wa madini ya ujenzi kama mawe. | Kamati inashauri eneo hili yasijengwe tena majengo ya chini na badala yake yaanze kujengwa majengo ya ghorofa. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 8. | 2.1.7 Mradi wa Marekebisho ya sehemu korofi katika Barabara ya Ndesingawa na Mahakama Abumalya hadi mzunguko wa sabasaba katika Manispaa ya Moshi (Namba 4170 (S10/009/2023/2024/W/09)) | Halmashauri ya Manispaa ya Moshi | Hadi wakati Kamati inatembelea mradi ulikuwa umekwisha kukamilika kwa asilimia 100, na kwamba uko katika muda wa maangalizi. | Kamati ilitaarifiwa kuwa mradi haukuwa na changamoto yoyote wakati wa utekelezaji wake | Kamati inaipongeza TARURA Mkoa wa Kilimanjaro kwa utekelezaji mzuri wa mradi huu. |
| 9. | 2.1.8 Mradi wa Ujenzi wa jengo la Utawala, Mionzi, jengo la kufulia na jengo la | Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vijijini | Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu ulikuwa umetekelezwa kwa asilimia zaidi ya 65 | Hali ya hewa- mvua nyingi zilizonyesha kwa muda mrefu zilisababisha Ubovu wa barabara hali iliyopelekea vifaa kutofika eneo la mradi kwa wakati; | Halmashauri kutekeleza miradi kwa kujenga mahusiano mazuri na watoa huduma ili kuweka maingira bora ya majadiliano na mapatano (negotiations) |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | dawa katika Hospitali ya Wilaya - Moshi (Mradi Namba 5401) | | | Kukwama kwa baadhi ya malipo kutokana na changamoto za mfumo wa malipo (MUSE) ambapo kutokana na changamoto hii, fedha zilipokelewa lakini mfumo ulikuwa hauwezi kulipa kwa muda mrefu na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa Mradi;<br><br>Mvua zinazoendelea kunyesha zimekuwa zikizuia mafundi kuendelea na ujenzi na hivyo kutishia ucheleweshwaji wa mradi huu. | Halmashauri ya Moshi kuongeza kiwango cha usimamizi ili kuharakisha ujenzi kama ilivyopangwa;<br><br>Mvua zinazoendelea kunyesha zinatishia kuharibu kabisa barabara na hivyo kuleta ugumu kwenye usafirishaji wa vifaa kwenda eneo la ujenzi. Kamati inashauri Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kununua vifaa kwa ujumla (bulk procurement) na kuviweka site ili kuondoa usumbufu wa usafiri mara itakapotokea barabara kuathiriwa na mvua nyingi zinazoendelea kunyesha. |
| 10. | Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Makoa | Halmashauri ya Wilaya ya Moshi | mradi huu ulianza Mtekelezwa tarehe 03 | Uwepo wa miamba maeneo barabara inakopita. Hali hii imesababisha kazi | Kamati inendelea kusisitiza Serikali kufanya upembuzi yakinifu wa kina katika |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Darajani – TACRI – Mferejini (7.0km) kwa Kiwango cha Lami Nyepesi (MSD) | | Novemba, 2022 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 25 Aprili, 2024. Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu ulikuwa umeshatekelezeka kwa asilimia 44 | kuwa ngumu na hivyo kuchelewesha utekelezaji;<br><br>Uwepo wa udongo laini maeneo barabara inakojengwa. Hali hii imesababisha ugumu wa utekelezaji wa mradi wakati wa ujenzi. | utekelezaji wa miradi mbalimbali;<br><br>Kutokana na kuongezeka kwa gharama za ujenzi, kinyume na maoteo, Kamati inashauri Serikali kuongeza fedha ili ujenzi wa kilometa 7.2 uweze kukamilika. |
| 11. | Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari Saashisha – Halmashauri ya Wilaya ya Hai (Mradi Namba 4390) | Halmashauri ya Wilaya ya Hai | Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu umekamilika kwa asilimia 100. inatembelea mradi ulifikia | Kamati ilitaarifiwa kuwa hapakuwa na changamoto yoyote wakati wa utekelezaji wa mradi huu. | Hapakuwa na maoni kuhusu utekelezaji wa mradi huu |
| 12. | Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Kupumzikia | Halmashauri ya Jiji la Tanga | Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu | Uwepo wa shida ya mifumo ya malipo ambapo malipo yalichelewa, hali | Serikali ichague eneo lingine la ujenzi wa jengo la kupumzikia viongozi wa kitaifa ambalo litakuwa na |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika Wilaya ya Tanga (Rest House) (Mradi Namba 6212) | | ulikuwa umeshafikia zaidi ya asilimia 85 | iliyosababisha kuchelewa kwa upatikanaji wa vifaa pamoja na malipo ya mafundi.<br>Uwepo wa hali ya hewa ya mvua ambayo ilisababisha shughuli za ujenzi kusimama katika baadhi ya siku. Hatua hii ilisababisha Halmashauri kuongeza mkataba wa mafundi kwa muda wa miezi mitatu. | ukubwa wa kutosha ili kuwapa viongozi hao nafasi na usalama wa kutosha wanapokuwa katika ziara mbalimbali za kikazi Jijini Tanga;<br><br>Serikali ilitumie jengo linalojengwa sasa, pale litakapokamilika, kwa shughuli nyingine ili liweze kuingiza mapato,<br>Ikiwa Serikali inahitaji kuendelea na eneo hilo basi Serikali inunue maeneo ya viwanja vya jirani ili kuliongezea ukubwa eneo linalojengwa nyumba hiyo. |
| 13. | Mradi wa Ujenzi wa miundombinu ya shule mpya ya Sekondari Kiomoni (Mradi Namba 4390 | Halmashauri ya Jiji la Tanga | Hadi wakati Kamati inatembelea mradi ulifikia zaidi ya 90 | Kamati ilitaarifiwa kuwa hapakuwa na changamoto zozote zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi huu. | Hapakuwa na maoni ya Kamati |